# Hongera kwa Kunde: Matumaini ya Mchango wa Nafaka katika Udhibiti wa Usalama wa Chakula

na  Nteranya Sanginga

**Nteranya Sanginga ni Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki**

**IBADAN, Nigeria, Januari 5 2016 (IPS)** - Mwaka wa 2016 ni Mwaka wa Kimataifa wa Kundi la Nafaka Zilizokaushwa, na sisi katika Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki (International Institute of Tropical Agriculture) tunafurahia kuandaa kongamano lijulikanalo kama Kongamano la Pamoja la Kimataifa na Afrika Nzima la Utafiti wa Nafaka Kutoka Jamii ya Kunde (Joint World Cowpea and Pan-African Grain Legume Research Conference).



***Nteranya Sanginga, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi Ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki (International Institute of Tropical Agriculture - IITA). Picha ni kwa hisani ya IITA***

Kongamano hili ambalo litaandaliwa nchini Zambia litawaleta pamoja wataalamu kutoka bara la Afrika na wataalamu kutoka sehemu zingine za dunia na kutoa fursa kwa wataalamu hawa kubadilishana mawazo kuhusu kundi la nafaka la mbegu zinazoliwa likijumuisha - kunde, maharagwe ya kawaida, dengu, nafaka ya chickpea, faba na maharagwe ya lima na aina mbalimbali za nafaka zenye mbegu zinazoliwa – kundi hili la nafaka litapewa fursa ya kuzungumziwa kama nafaka yenye virutubishi vyenye manufaa zaidi.

Kundi la Nafaka Zilizokaushwa huwa na mbegu ambazo huchukuliwa kuwa ni ndogo kwa ukubwa, lakini kundi hili la nafaka lina umuhimu sana kiafya.

Wataalamu wa lishe wametambua mara kwa mara kwamba viwango vya chini vya gilaisemiki katika nafaka hizi na viwango vya juu vya faiba husaidia kuzuia na kudhibiti magonjwa yanayotokana na mienendo ya maisha kama vile magonjwa yatokanayo na utajiri kwa mfano kunenepa sana na kisukari. Na protini katika nafaka hizi huwa na uwezo mkubwa wa kusaidia wafugaji duniani kudhibiti mbinu za ufugaji wanyama kwa njia endelevu na ya kudumu, uendelevu huu utawasaidia watu wengi kuendelea kufarahia zaidi nafaka na kuwepo kwa mlo kamili kwa watu wenye mapato ya wastani bila kuathiri zaidi rasilimali asilia.

Kwanza kabisa, lazima tuunde mikakati ya kuwezesha uwepo wa nafaka katika Kundi la Nafaka Zilizokaushwa kupatikana kwa wengi. Uwezo wa Kijumla wa uwepo wa Kundi la Nafaka Zilizokaushwa duniani umepungua kwa zaidi ya thuluthi moja katika miongo minne iliyofuata miaka ya 1960.  Lakini kuanzia mwaka wa 2005, uzalishaji wa nafaka katika Kundi la Nafaka Zilizokaushwa umeendelea kuongezeka kwa kasi, hasa katika mataifa yanayoendelea. Nafaka ya kunde imekuwa mojawapo ya

ongezeko la nafaka katika Kundi la Nafaka Zilizokaushwa, kunde imeonyesha ongezeko katika mazao yake na pia ongezeko la hektari ambazo nafaka ya kunde inapandwa.

Kimsingi, karibu asilimia 20 ya nafaka zote ulimwenguni huuzwa, ongezeko hili ni angalau mara tatu ya uuzaji wa nafaka kutoka Kundi la Nafaka Zilizokaushwa kutoka mwaka wa 1980. Ukuaji wa biashara ya nafaka katika kundi hili hautoshelezi kiwango cha ukuzaji wa nafaka kutoka Kundi la Nafaka Zilizokaushwa. Zaidi ya hayo, Amerika Kaskazini ina nafasi kubwa ya uuzaji wa nafaka kwa mataifa mengine, kama ilivyo Afrika Mashariki na Myanmar: zaidi ya nusu ya mauzo ya nafaka zilizokaushwa kwa mataifa mengine sasa yanatoka katika mataifa yanayoendelea.

Kuna nafasi kubwa ya kukuza zaidi vyanzo vya protini kutoka nafaka hizi.

Habari njema kwa mamilioni ya wakulima wadogo ni kwamba nafasi ya ukuaji huu wa nafaka zilizokaushwa sio tu mchango katika kukuza thamani ya kitamaduni ya nafaka bali pia ni mageuzi katika maisha ya lishe ya mwanadamu. Thamani ya kijadi ya nafaka zilizokaushwa inatiliwa mkazo na mfanyabiashara mashuhuru wa Kiarabu Ibn Battuta alipokuwa kwenye safari ya kuelekea Mali na Sahel katika mwaka wa 1352, alipoandika kuhusu kokwa ya Bambara iliyokaangwa katika mafuta ya shea. Mara nyingi, mabaki ya kunde yajulikanayo kama akara nchini Nigeria huonekana katika vibanda barabarani katika eneo la Afrika Mashariki kote, mabaki haya ndiyo chanzo asilia cha nafaka kutoka jamii ya kunde. Kundi lingine lenye uhusiano na kunde la acarajés, lilitangazwa kama sehemu ya utamaduni asilia wa Brazili- ambapo nafaka ya acarajés huliwa pamoja na nduvi - na jina lake la Yoruba halikupotea kutokana na biashara ya utumwa**.**

Katika Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki (IITA) tumekuwa tukikuza nafaka ya kunde kwa miongo mingi. Mwezi huu, Wizara ya Kilimo ya Swaziland iliwapa wakulima mbegu mpya ambazo tumekuwa tukitayarisha- mbegu ambazo hukua haraka kwa asilimia 20 na zenye mazao ya mara nne zaidi ya mbegu za awali. Mafanikio haya ya hivi majuzi yana umuhimu sana, shukrani kwa hifadhi ya mbegu ya Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki (IITA). Hifadhi hii ina aina 15,112 ya mbegu maalum mbalimbali za kunde kutoka mataifa 88.

Kwa nini idadi hii kubwa ya mbegu za kunde? Swali letu ni kwamba, kwa nini mbegu zaidi za kunde hazipandwi!

Kwa kuwa, kunde ina asilimia 25 ya protini, kupanda kunde ni mbinu nzuri ya kuupa udongo vitamini na madini, kunde huweza kupandwa katika udongo wa aina mbalimbali, kunde huweza kuhimili ukame na pia kivuli, kunde hukua kwa haraka ili kukabili mmomonyoko wa udongo na kunde pia huupa udongo naitrojeni. Tunaweza kula mazao kuu ya kunde – yajulikanayo kama kokwa zenye rangi nyeusi-na wanyama hufurahia vijiti na majani yake.

Basi kwa nini hatusikii kuhusu kunde? Labda ulimwengu haukuwa unafahamu umuhimu wa kunde, lakini sasa kunayo fursa nyingine ya dunia kubadilisha hali hii.

Kimsingi, kunde huwa na matatizo wakati wa ukuzaji wake. Kwanza, mmea huu unaweza kuangamizwa katika hatua yoyote ya ukuaji wake, iwe kutoka kwa vidudu vya afidi, virusi vya mosaiki, vichimba

mbegu, magugu makali, au wadudu walao nafaka wanaoogopwa zaidi ambao hupigana na fungi kwa kutumia fungi na bakteria na kuzila mbegu zilizohifadhiwa. Haya ndiyo mambo wanasayansi wa Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki (IITA) wanajaribu kukumbana nayo, kupitia uzalishaji mbegu na uenezi wa teknolojia vumbuzi kama vile begi za PIC ambazo hukinga wadudu wanaokula nafaka.

Kuna mengi ya kujifunza kuhusu mmea wa kunde, miongoni mwa haya ni pamoja na  jinsi ya kuukuza, na jinsi ya kuboresha nafasi yake katika mfumo wa chakula. Ninaunga mkono kwamba watu wataweza kujifunza mengi kuhusu uchakataji nafaka ya kunde, hatua muhimu ambayo inawaruhusu wafanyabiashara wengi Wanigeria kufanikiwa zaidi katika Mwaka huu wa Kundi la Nafaka Zilizokaushwa. Angalau watengenezaji wa kimataifa wa vyakula watagundua mbinu mpya za kusiaga bidhaa za nafaka ili kuzalisha vyakula vyenye afya zaidi na vyenye protini kamili.

Kwa upande wa ukulima wa kunde, mmea huu unaweza kupunguza magugu mashambani na kuwa mbolea ya mazao ya biashara. Pia mmea huu wa kunde huvunwa kama nafaka, na hali hii huleta usalama na udhabiti wa usalama wa chakula na ukiwapa wakulima uwezo wa kuchagua kuwachilia mmea huu kukua huku ukipunguza mazao ya maharagwe na kuongeza mazao ya foda.

Kijenetiki na kufikia hivi leo- Kitovu cha mmea huu- ni eneo la Afrika Mashariki. Nigeria ndiyo nchi inayotoa mazao makubwa zaidi ya kunde duniani lakini pia huwa ni mnunuzi muhimu katika ununuzi wa mazao ya mmea huu kutoka mataifa jirani. Nchi ya Niger ndiyo nchi inayouza mazao zaidi ya kunde duniani kote. Lakini uwezo wa kunde kukumbana na hali ya anga ambapo hakuna mvua na mmomonyoko wa udongo unaweza kuibua ari ya kukuza kunde katika sehemu nyinginezo za ulimwengu kwa mfano sehemu zenye jua kali huko Amerika Kaskazini.

(Mwisho)